*JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA*

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA.**


Shule ya Sekondari Rugambwa,
S.L.P. 357,
**BUKOBA.**
**Novemba, 2025.**

**Namba za Simu**
Mkuu wa Shule- 0623-610088
Makamu Mkuu wa Shule- 0759813425
Matron – 0756882895
Mama Malezi – 0767665844 / 0786665616


**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI RUGAMBWA HALMASHAURI YA MANISPAA YA BUKOBA MKOA KAGERA MWAKA 2026**

Ndugu Mzazi/Mlezi,

Ninafurahi kukutaarifu kuwa binti yako ……………………………………………………….. amechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha kwanza kwa mwaka 2026. Kwa niaba ya jumuiya ya Shule ya Sekondari Rugambwa, ninampongeza kwa mafanikio hayo na vile vile namkaribisha shuleni hapa.

Shule ya Sekondari Rugambwa ipo umbali wa kilometa 5 toka Bukoba mjini, usafiri wa teksi unagharimu kiasi cha Tsh. 7,000/= hadi 8,000/= na usafiri wa pikipiki ni shilingi kati ya Tsh. 1500/= hadi Tsh. 2000/=

Mkoa wa Kagera unawasiliana na mikoa mingine kwa barabara, meli na anga. Mzazi ana uchaguzi wa njia ya kutumia.

1.0. **KUFUNGUA SHULE:**

Shule itafunguliwa tarehe **13.01.2026** binti yako anapaswa kuwahi kozi ya Kiingereza itakayoanza mara moja baada ya kufungua, akichelewa sana hatapokelewa na nafasi yake atapewa mwanafunzi mwingine.

2.0. **MAHITAJI:**

Binti yako alete vifaa vifuatavyo anapokuja kuanza shule:-

(a) **VIFAA VYA DARASANI:**

(i) Madaftari makubwa yasiyopungua 12

(ii) Mkebe wa Hisabati (Mathematical set)

(iii) Rula, Kalamu za wino na penseli za kutosha muhula

(iv) Dictionari ya kingereza kwa kingereza.

(v) Ream 1(double A)

(b) **<u>SARE YA SHULE (UNIFORM)</u>**

(i) Shati nyeupe 2 zenye mikono mifupi aina ya tomato na zisizo na urembo wowote. (siyo **halua**)

(ii) Soksi nyeupe jozi 4, Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi, vyenye kufunika miguu na kufungwa kwa kamba na visivyo na urembo wowote (**siyo mfano wa buti**) jozi 2

(iii) Nguo za michezo "track suit"ya rangi ya kijani jeshi (**dark green**) iliyokolea na yenye kitambaa Kizito isiwe ya kubana mwili na isiyofunika kichwa, fulana na kaptula lake linalofika kwenye magoti (jezi) rangi ya kijani jeshi **(dark green)** na raba nyeupe jozi 1. **Rejea picha inayoonesha rangi husika.**

(iv) Sweta rangi ya kijivu shingo la "V" yenye michirizi myekundu miwili shingoni, mikononi na kiunoni yenye nembo ya shule.

**(picha imeambatanishwa)**

(v) Tai yenye michirizi myeupe na myeusi. **(picha imeambatanishwa)**

(vi) Sketi nyekundu mbili (2), kitambaa kizito (Esteem) yenye mshono wa

"malindabox" jumla ya malinda yawe kumi, mbele matano (5) na nyuma matano (5) na michirizi miwili ya kitambaa cheupe cha tetron inalala kwenye linda la katikati mbele. Upana wa mchirizi ni nusu inchi na nafasi kati ya mchirizi na mchirizi ni nusu inchi. Sketi iwe ndefu ya kufunika miguu hadi kwenye kifundo cha chini cha mguu **(picha imeambatanishwa).**

(vii) Rangi ya hijab (kijuba) ni nyeupe na nyeusi ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama **(Picha imeambatanishwa).**

(viii) Nguo za nje ya darasa (shamba dress)

- Gauni 2 rangi ya kijani jeshi (dark green) iliyokolea kitambaa cha tetron nzito au esteem. Iwe ndefu hadi kwenye kifundo cha chini cha miguu, mshono wa solo mikono mirefu. **Rejea picha inayoonesha rangi husika.**
- "T-Shirt" rangi ya njano iliyoiva yenye shingo ya duara kitambaa kizito **(siyo babalance) yenye nembo ya shule. (picha imeambatanishwa)**

Picha kuhusiana na sare za shule zimeambatanishwa, tafadhali rejea kwenye picha hizo. Aidha, ukipata mkanganyiko piga simu kwa kutumia namba zilizotajwa.

**TANIBIHI:** Mwanafunzi aje amevaa mojawapo ya sare za shule tajwa hapo juu, **asije na nguo yoyote ya nyumbani.**

### (c) MAHITAJI BINAFSI KWA MATUMIZI YAKE:

- Mwavuli wa mvua 1
- Mto mmoja na foronya 2 za rangi ya pinki **zisiwe na urembo**
- Mashuka manne (4) rangi ya pinki **yasiyo na urembo** na blanketi 1
- Godoro moja la futi 2½ lililovalishwa mpira wa mkojo hata kama hakojoi kitandani, nguo za kulalia (**Night dress**) 2, kanga au kitenge jozi moja.
- Sahani 1, bakuli 1, kikombe1, kijiko 1, vyombo vyote viwe vya bati.
- Toilet papers (karatasi za chooni) 10
- Kifaa cha kutunzia maji ya kunywa (dumu la lita 3 au 5)
- Taulo 1
- Nguo za ndani (gagulo 2, chupi zisizopungua 6 na sidiria 3),
- Pedi (always paketi 4) hata kama hajaingia kwenye hedhi.
- Dawa ya viatu na brashi, mafuta ya kupaka na kitana, sabuni, mswaki na dawa ya meno.
- Fedha za matumizi binafsi. Shule hutoa chakula, mpatie binti yako fedha kiasi kwa matumizi yake ya kawaida awapo shuleni. Fedha nyingi humfanya ashindwe kufuatilia masomo ipasavyo. (fedha hizi zitatunzwa kwa mhasibu wa shule)
- Ndoo 1 ya kuchotea maji yenye ujazo wa lita 20.
- Beseni la kuogea 1
- Chandarua 1 kwa ajili ya kuzuia mbu

**MUHIMU: Mzazi/mlezi hakikisha vifaa vyote vya mwanao vimewekewa alama inayoonekana ili kuzuia upotevu.**

### (d) MAHITAJI MENGINE:

(i) **Matibabu** - Ni jukumu la mzazi, kuhakikisha mtoto wake ana bima ya afya hivyo, kila mtoto lazima aje na bima ya afya inayotambulika**.** Kama mwanao **HANA BIMA** ya afya utapaswa kulipa **Tsh. 50,400/=** ili akatiwe **BIMA**. Fedha hiyo italipwa kwenye taasisi inayoshughulika na bima kupitia kwa mhasibu wa shule.

(ii)Picha mbili za mwanafunzi (passport size), moja ibandikwe kwenye fomu anayokuja nayo shuleni na ya pili itabandikwa kwenye jalada atakalofunguliwa shuleni.

(iii) Aje na hard broom (brashi ngumu yenye mpini ya kusugulia sakafu) moja na mifagio miwili ya nje (chelewa).

## 3.0. MAMBO MUHIMU YA KUFANYA KABLA YA KURIPOTI SHULENI:

Binti yako atatakiwa kukamilisha fomu zilizoambatanishwa na kuleta vitambulisho /uthibitisho kama ifuatavyo:

(i) **Fomu ya afya (Medical Examination form**)

Ni lazima binti yako apimwe katika hospitali ya serikali na daktari au mganga mkuu na kukamilisha vipengele kuhusu afya yake. Fomu hii lazima iwasilishwe shuleni mara anapokuja kuripoti.

(ii) **Cheti cha uraia-** Alete cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate) au cheti cha utambulisho wa uraia, ambacho hupatikana kwa Mkuu wa Wilaya yako. Kumbuka hatutakubali utambulisho wa vijiji, Kata au Tarafa.

(iii) **Taarifa binafsi**: Fomu maalum imeambatanishwa. Fomu hii ijazwe kwa uangalifu na kurudishwa hapa shuleni anapokuja kuripoti.

(iv) **Fomu ya sheria za shule**, aje nayo ikiwa imesainiwa na mzazi pamoja na mwanafunzi ikiwa wamekubaliana na sheria za shule.

## 4.0 MAMBO MENGINE YA KUZINGATIA

Kuna likizo fupi mbili kwa mwaka. Wakati huu shule huruhusu wanafunzi kwenda nyumbani kwao.

Kuondoka bila ruhusa ni **utoro.**

Pia kuna likizo mbili ndefu. Hii pia kila mwanafunzi huruhusiwa kwenda nyumbani kwao. Shule huwaruhusu wanafunzi wote ili wasafiri kwenda kwa wazazi/walezi wao na siyo kwingineko. Ni jukumu la mzazi kuhakikisha ya kuwa umempokea mtoto wako na kumtunza inavyopaswa. Ni mategemeo ya shule kuwa wakati huo vijana watatumia muda wao vizuri kwa kuwasaidia wazazi kufanya shughuli mbali mbali za kuzalisha mali na kusoma, kuliko kuzurura ovyo.

Ni sheria ya shule kwamba baada ya likizo kila mzazi ahakikishe mtoto wake anawahi shuleni kwa tarehe iliyopangwa na analeta mahitaji yote muhimu. Akichelewa atalazimika kuja na mzazi/mlezi au barua ya mzazi / mlezi ikieleza sababu ya kuchelewa la sivyo atachukuliwa hatua za kinidhamu.

## 5.0 UTUMAJI WA FEDHA BINAFSI KWA MWANAFUNZI

Wazazi wanaowatumia watoto wao fedha za matumizi wafanye hivyo kwa kutumia namba za simu zifuatazo:

**M-PESA:0756 882 895 au Airtel Money: 0788885787 Sika Mwita Chacha (Matron)**

**0767 665 844 au 0786665616 – Mariana Jovinus Mugizi (Mama Malezi).** Taarifa za kuwataka wanafunzi kufuata fedha zilizotumwa kupitia kwa jamaa zao wanaokaa nje ya shule hazitakubaliwa. Hairuhusiwi mzazi/mlezi/ndugu **kuwasiliana au kutuma fedha** kwa mwanafunzi kwa kutumia namba za simu tofauti na zilizotajwa hapo juu.

**6.0. <u>MWISHO</u>**: Hakikisha umekamilisha mahitaji yote na kujaza fomu zote zilizoambatanishwa kabla ya kumleta mtoto shuleni: Fomu ya taarifa binafsi, fomu ya afya (Medical Examination form) na sheria za shule zilizotiwa sahihi.

**KARIBU SANA**

**WITNESS K. AMOS**
**MKUU WA SHULE.**

**JINA LA MWANAFUNZI ________________________________KIDATO CHA ___________**
**MWAKA______________**

**7.0 SHERIA ZA SHULE:**

Shule inazo sheria/taratibu zake za kuishi. Binti yako anapaswa kuzifuata na kuzitii taratibu hizo kama zilivyotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na zinavyosimamiwa na shule. Ni vizuri kuelewa kuwa iwapo taratibu hizi zitakiukwa basi shule inaweza kulazimika kumsimamisha masomo mwanao. Aidha miongoni mwa mambo ambayo yanayoweza kusababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na:-

(a) Wizi
(b) Uasharati
(c) Ulevi wa aina zote
(d) Makosa ya jinai
(e) Kuharibu makusudi mali ya Umma
(f) Kupata mimba na au kutoa mimba.
(g) Kuolewa
(h) Kulala nje ya shule bila ruhusa maalum.
(i) Kudharau Bendera ya Taifa.
(j) Uvutaji bangi/sigara
(k) Kupigana
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kukutwa na simu ya mkononi au laini ya simu au kiashiria chochote cha simu
(n) Kuanzisha au kuchochea migomo shuleni.

(i) **MWANAFUNZI AWAPO SHULENI HAPASWI KUFANYA YAFUATAYO:**

- Kufuga kucha ndefu
- Kupakaa rangi kwenye kucha, mdomo, kope au nyusi
- Kutumia vipodozi
- Kufuga nywele au kukata tofauti na maelekezo ya mwandamizi wa malezi na Utamaduni (mwanao atapaswa kuwa na nywele fupi zisizozidi 1cm.
- Kuvaa nguo fupi au zinazobana mwili.

(ii) **MWANAO AWAPO SHULENI ATATAKIWA.**

- Kuhudhuria vipindi vyote bila kukosa.
- Kuvaa sare ya shule /ya kazi wakati wote
- Kutii amri zote za shule
- Kujiheshimu, kuheshimu wenzake, viongozi na watu wote kwa ujumla.
- Kutunza mali zake na mali za umma.

(a) **HESHIMA**

- Mwanafunzi anatakiwa kusimama na kuamkia walimu, wafanyakazi wasio walimu pia mtu/mgeni yeyote anayemzidi umri anapopita na anapoingia darasani au kwenye ukumbi wa mikutano.
- Mwanafunzi kama kila raia mwema, lazima aheshimu Bendera ya nchi yake na wimbo wa Taifa.

- Matusi, lugha chafu na kupigana ni dalili ya kukosa heshima.

(b) **UTII**

- Kila mwanafunzi hana budi kutii na kufuata maelekezo na maagizo ya viranja, walimu na wafanyakazi wasio walimu.
- Mwanafunzi anapoitwa mahali lazima aitike, na kukimbia kule aliko kiongozi anayemwita.
- Kiburi, majibu ya jeuri na matumizi ya lugha mbaya haviruhusiwi.
- Ni wajibu kila mwanafunzi kufanya na kukamilisha kazi anayopangiwa iwe nje au ndani ya darasa

(c) **UPENDO**

Mwanafunzi ajipende yeye mwenyewe, na awapende wenzake kama ndugu zake wa shuleni, awapende walimu kama wazazi wake, aipende shule yake kama nyumbani kwake, aipende na kujivunia nchi yake ya Tanzania.

**(iii)RUHUSA**

Ruhusa maalum ya kutoka nje ya shule itatolewa mara moja kwa muhula (shopping day)

(iv) **MAMBO YA MSIBA**

Mwanafunzi akifiwa akiwa shuleni ataruhusiwa kuomboleza shuleni tu. Isipokuwa akifiwa na mzazi au mlezi ataruhusiwa kwenda nyumbani.Taarifa zote za kifo zipitie kwenye ofisi ya Mkuu wa Shule. Ruhusa ya kwenda nyumbani itatolewa na Mkuu wa Shule baada ya kuzingatia taratibu muhimu.

(v) **MABADILIKO YA ANWANI**:

Unashauriwa kutoa taarifa kwa Mkuu wa Shule iwapo anwani inayotumika kwa mawasilino imebadilika.

(vi) **RIPOTI ZA MAENDELEO KITAALUMA**

Shule hutuma taarifa za maendeleo ya mwanafunzi kitabia na kitaaluma kila muhula. Tafadhali hakikisha unaipata, na kutuma maoni yako shuleni.

JE UNAKUBALI? **NDIYO** ☐ **HAPANA** ☐

(Weka alama ya √ panapohusika)

Jina la Mwanafunzi________________________ Sahihi _______ Tarehe ____________

Jina la Mzazi _________________ _________ Sahihi _______ Tarehe __________

ANUANI YA MZAZI

…………………………………………….
.

…………………………………………..

**TAARIFA BINAFSI**

A:Jina la Mwanafunzi ......................................................................................................
Anwani ya nyumbani ...........................................................................................

...............................................................................................................................
........ Kabila ........................................ Tarehe aliyozaliwa ......../........../.........
Mtanzania /Si Mtanzania

Dini ya Mwanafunzi....................... Mtaa/Kijiji …………… Kata ……………..Jina la mratibu elimukata/mtendaji……………………..Namba ya simu……..………Wilaya.....................Mkoa..................

B. Jina la baba ................................................. * (Hai/Marehemu) .................(Mwaka aliofariki)

Dini ya baba ................................. Kazi ya baba ............................... Na. simu ……………........

Jina la Mama .....................................................*(Hai/Marehemu) ...............(Mwaka aliofariki)..........

Dini ya Mama ............................... ................ Kazi ................................. Na. ya simu.…......................

C. Taja majina na anuani za Walezi/Ndugu wengine wawili wasiokuwa wazazi wanaoruhusiwa kufika shuleni kusikiliza na kutoa maamuzi juu ya mashauri ya mtoto wako.

Jina .........................................Uhusiano ………… …..Umri ............................ Na. simu....................

Jina ..........................................Uhusiano …………….Umri ............................ Na. simu....................

D. Taja majina ya watu watakaoruhusiwa kumtembelea mtoto wako akiwa hapa shuleni.

1. .......................................Uhusiano .....................Umri.............Anuani……….Na. simu …………

2. .....................................Uhusiano ....................Umri...............Anuani………Na. simu…………..

3. ......................................Uhusiano .....................Umri...............Anuani………Na. simu …………

**A.picha za wazazi**

| | |
|---|---|
| | |

**B.picha za walezi wawili**

| | |
|---|---|
| | |

## MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY

## FORM FOR STUDENT MEDICAL EXAMINATION

Student's Name ………………………………………………………………………………

Blood Examination: Haemoglobin …………………………Blood Group ………………………

Stool Examination ……………………………………………………………………………

Urinalysis ………………………………………………………………………………………

Pregnancy test …………………………………………………………………………………

T.B. Test (If negative, was immunization given) ……………………………………………
Eyes ……………………………………………………………………………………………
Chest ……………………………………………………………………………………………
Any chronic complaints not noted above e.g.

Asthma …………………………………………………………………………………………
Headache ………………………………………………………………………………………

Inability to eat certain foods …………………………………………………………………

Skin diseases etc ………………………………………………………………………………

Also, anything that the School health staff should know about…………………………………………….

Any treatment given or recommended …………………………………………………………

**NOTES**: If any of the examinations requested above cannot be carried out, it is useful if it is noted that they have not been done rather than writing NAD down. In case of Bilharzia it is recommended that students attend the Bilharzia clinic before they come to school.

Signature of Examiner ………………………….

Designation …………………………………….
Date ……………………………………………. Station ………………………………









